JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

Mtaa wa Mwenge,
S.L.P. 588,
54201 Mbozi - Songwe.
Simu: (025) 2580226
Nukushi: (025) 2580213
Barua pepe: rbcsongwe@pccb.go.tz
Wavuti: http://www.pccb.go.tz

TAARIFA KWA UMMA

SONGWE - JANUARI 10, 2019

TAKUKURU MKOA WA SONGWE YAMKAMATA ALIYEKUWA MHANDISI WA MAJENGO HALMASHAURI YA SONGWE KWA RUSHWA

Ndugu Wanahabari;

Ofisi ya TAKUKURU Mkoa wa Songwe kwa kipindi cha Oktoba - Disemba 2019 imemkamata aliyekuwa Mhandisi wa Majengo Halmashauri ya wilaya ya Songwe kwa kwa Rushwa. Mhandisi huyu kwa sasa anafanya kazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama mkoani Singida.

Tukio hili lilitokea mnamo tarehe 30 mwezi Disemba, 2019 katika eneo la Mkwajuni, Halmashauri ya wilaya ya Songwe, kwamba aliyekuwa Mhandisi wa Halmashauri ya Wilaya ya Songwe Ndg. CRYRILLE AUGUSTINE MKOMBOZI aliomba hongo ya Shilingi 200,000/= toka kwa mwananchi aliyekuwa akitaka kibali cha ujenzi na kupokea kiasi cha Shilingi 150,000/= kwa njia ya M-Pesa. Mnamo tarehe 29.12.2019 alipokea kiasi cha Shilingi 70,000/= kupitia simu yake ya mkononi namba 0767-526950 na tarehe 30.12.2019 alitumiwa kiasi cha Shilingi 80,000/= kupitia simu ya mtu mwingine aliyekuwa mtumishi mwenzake.

Fedha hizo za hongo zilizoombwa na kupokelewa na Mhandisi huyu zilikuwa ni kwa ajili ya kumpatia kibali cha ujenzi Mkazi huyo wa Mkwajuni ambaye alillipia kibali hicho jumla ya Shilingi 300,000/= na kupatiwa stakabadhi, lakini hakupatiwa kibali chake cha ujenzi, japo aliruhusiwa kuendelea na ujenzi huo. Aliyekuwa akishughulikia utolewaji wa kibali hicho ni Mhandisi MKOMBOZI. Baada ya kumaliza ujenzi na kufika Halmashauri ya wilaya ya Songwe ili kupata leseni ya biashara, ndipo alitakwa kuonyesha kibali cha ujenzi ambacho hakuwa nacho. Baada ya kuwasiliana na Mhandisi MKOMBOZI ndipo walipokutana kwa kuwa kipindi hicho Mhandisi MKOMBOZI alikuwa Mkwajuni

Songwe kwa shughuli zake, walipokutana na Mkazi wa Mkwajauni ndipo alimuomba hongo hiyo ya Shilingi 200,000/=

Ofsi yetu ya TAKUKURU Wilaya ya Songwe ilipata taarifa na ilifanya ufuatiliaji kufanikiwa kumkamata Mhandisi MKOMBOZI ambaye alipokea Shilingi 70,000/= kwenye simu yake ya mkononi, pia kiasi cha Shilingi 80,000/= zilitumwa kwa aliyekuwa mtumishi mwenzake na Mhandisi MKOMBOZI ambaye alitumiwa fedha hizo kwa niaba ya Mhandisi MKOMBOZI. Uchunguzi umefanyika na kukamilika, tayari Mhandisi MKOMBOZI amefikishwa katika Mahakama ya Mkoa wa Songwe kujibu mashtaka yanayomkabili.

Ndugu Wanahabari;

Katika kipindi husika, Ofisi yetu pia iliendelea na majukumu yake mengine ambapo katika Uchunguzi na Mashitaka Ofisi yetu ilipokea jumla ya taarifa 40 za malalamiko ya vitendo vya rushwa. Kati ya malalamiko hayo, malalamiko 17 (42.5%) yalipokelewa toka kwa wananchi kwa kufika ofisini moja kwa moja kuleta kero zao; malalamiko 11 (27.5%) yalipokelewa kwa njia ya barua; malalamiko 6 (15%) yalipokelewa toka vyanzo vingine; malamiko 5 (12.5%) yalipokelewa kwa njia ya simu na lalamiko 1 (2.5%) lilipokelewa kwa njia ya barua pepe.

Aidha Ofisi yetu imeweza kuokoa fedha jumla ya ~~Tshs.~~ 300,374,673.40 fedha hizo zimeokolewa toka Vyama vya Ushirika (AMCOS. Fedha hizi zilikopwa na AMCOS toka Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) ambazo zilitakiwa kurejeshwa kwa msimu wa kilimo kwa mwaka 2017/2018 pamoja na 2018/2019 lakini hazikurujeshwa kwa wakati.

Katika uelimishaji Umma kuhusu rushwa na madhara yake Ofisi yetu iliendelea kuelimisha makundi mbalimbali ambayo ni Wanafunzi, Vijana, Wanawake, Wanachama wa Vyama vya Siasa pamoja na Watumishi wa Mashirika ya Umma na Mamlaka nyingine za Serikali zilizo katika Mkoa wetu. Katika kipindi cha Octoba - Disemba 2019 imeweza kufanya jumla ya Mikutano 121; Semina 61; Ufunguaji na Uimarishaji wa Vilabu vya Wapinga rushwa 110; Uandishi wa Makala 04 pamoja na Maonesho 03.

Vilevile Ofisi yetu imeweza kutembelea na kukagua miradi 10 ya maendeleo yenye jumla ya thamani ya Tshs. 10,532,059,130/= Miradi iliyotembelewa ni ujenzi wa soko la Kimataifa la mazao na Mifugo Kakozi unaotekelezwa kwa *"Force account"* yenye thamani ya Tshs. 8,645,000,000/=; Matengenezo ya kipindi Maalum na ya Kawaida ya barabara ya Kakozi - Ilonga wenye thamani ya Tshs. 197,887,000/=; Ujenzi wa daraja la Msisiwe lililopo kata ya Mpemba H/Mji Tunduma wenye thamani ya Tshs. 43,881,300/= Ukamilishaji wa jengo la OPD zahanati ya Katete Mpemba weneye thamanai ya Tshs. 32,375,000/=; Ujenzi wa daraja barabara ya Chang'ombe Insani wenye thamani ya Tshs. 93,119,000/=; Ujenzi wa vyumba vya madarasa na mabweni Shule ya sekondari Msia wenye thamani ya Tshs. 196,000,000/=; Ujenzi wa vyumba vya madarasa na mabweni Shule ya sekondari Myovizi wenye thamani ya Tshs. 196,000,000/=; Ujenzi wa barabara

ya Itumba - Isongole wenye thamani ya Tshs. 182,274,500/=; Mradi wa Ujenzi wa Shule ya Sekondari Luswiswi wenye thamani ya Tshs. 141,000,000/=; na Mradi wa uboreshaji huduma ya Maji Itumba - Isongole wenye thamani 804,162,330/=. Miradi yote inaendelea vizuri isipokuwa mradi wa ujenzi wa Shule ya Sekondari Msia kufuatia wananchi wa kata ya Msia kutoshiriki kikamilifu katika shughuli za ujenzi huo. Pia tumefanya Warsha katika Ukusanyaji wa Mapato kwa kutumia Mashine za Mfumo (PoS) kwenye kila Halmsahuri katika mkoa wa Songwe.

Ndugu Wanahabari;

Ofisi yetu kwa kipindi cha Januari - Machi 2020 imejipanga kufuatilia fedha za Vyama vya Ushirika (AMCOS) ambazo walikopa lakini bado hawajarejesha kwenye benki mbalimbali pamoja na fedha wanazodaiwa na wananchi. Pia kufuatilia mali za AMCOS ambazo zimebinafsishwa na watu wachache kwa manufaa yao binafsi. Sambamba na ufuatiliaji wa fedha za AMCOS, katika kipindi hiki tutatoa elimu ya rushwa katika Kuhamasisha Kampeni ya UTATU na TAKUKURU APP ambazo zitajikita kutatua changamoto za rushwa barabarani ,jinsi ya kutolea taarifa vitendo vya rushwa na Rushwa ya ngono.

Ndugu Wanahabari;

Tunawashukuru sana kwa ushirikiano wenu mnaouonesha kwa Ofisi yetu hususani kwa kutuletea taarifa za vitendo vya rushwa pindi mnapovisikia. Nipende kutoa rai kwa viongozi wote wa Vyama vya Ushirika (AMCOS) kuhakikisha kuwa fedha zote wanazodaiwa na benki mbalimbali pamoja na wanazodaiwa na wananchi wahakikishe zinawafikia wahusika kabla Ofisi yetu haijawafikia wao. Nitoe wito kwa wananchi kuendelea kutupatia ushirikiano ili kwa pamoja tutokomeze vitendo vya rushwa ambavyo vinaendelea katika maeneo yetu.

Ninawakushukuru nyote kwa kufika na kunisikiliza, ninaamini mtaifikisha taarifa hii kwa wananchi pamoja na watumishi wa umma ili kila mmoja atambue wajibu wake katika mapambano haya kwa ustawi wa maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika Taifa letu.

Damas Suta,
Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Songwe